


- Kutoa miongozo juu ya ununuzi wa vifaa vyote vya TEHAMA katika Utumishi wa Umma
- Kuhakikisha usalama wa TEHAMA katika Utumishi wa Umma unalindwa na kuhifadhiwa
- Kusimamia mfumo wa barua pepe wa serikali.
- Kusanifu tovuti pamoja na kuzihifadhi (web hosting)
- Kujenga uelewa kwa wananchi juu ya huduma zinazotolewa kupitia Serikali
- Kutoa ripoti juu ya maendeleo ya utekelezaji wa Serikali Mtandao na mafanikio yake kwa Serikali na jamii kwa ujumla.



Idara ya Serikali Mtandao Zanzibar

Uimarishaji TEHAMA katika taasisi za Umma



Mawasiliano

Idara ya Serikali Mtandao

Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora
Mtaa wa Mazizini, Jengo la Katiba Ghorofa ya Saba
S.L.P 1333, Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 22 35688 Nukushi: +255 24 22 35689

Barua pepe: info@egoz.go.tz

Tovuti: www.egoz.go.tz

Nini Serikali Mtandao?

Serikali Mtandao (e-Government) ni utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa Serikali katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Idara ya Serikali Mtandao

Ni idara ilioundwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na. 2 ya mwaka 2011 kifungu namba 97 na kuipa jukumu la kusimamaia masuala ya TEHAMA ndani ya serikali ili kutekeleza kazi zake.

Dira

Kuwa na serikali mtandao yenye ufanisi na uhakika kwa utawala bora Afrika.

Dhamira

Kutoa huduma bora kwa umma na kukuza utawala bora ulio endelevu kwa kutumia TEHAMA iliyo salama na yenye kuaminika.

Malengo Makuu

- **Kuandaa sera za TEHAMA pamoja na kusimamia utekelezaji ndani ya utumishi wa umma.**

Idara inaandaa sera mbali mbali za TEHAMA kama vile sera ya serikali mtandao (egovernment policy) ili kuwa na matumizi sahihi ya TEHAMA katika utumishi wa umma.

- **Kutoa miongozo na kanuni za TEHAMA ndani ya serikali**

Idara ya Serikali Mtandao inaten geneza miongozo na kanuni ili kusimamia udhibiti wa viwango vya mambo mbali mbali yanayohu siana na TEHAMA.

- **Kuhamasisha uwezo wa Taasisi za Serikali katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA**

Idara inatoa mafunzo mbali mbali, kuzishauri Taasisi za umma pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wake katika kuzifikia jitihada za Serikali mtandao.

- **Kuimarisha huduma za ushauri wa kitaalamu**

Idara inatoa huduma ya ushauri wa kitaalamu katika taasisi za umma, miongoni mwa huduma hizo ni ushauri juu ya ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA, utengezaji na uendeshaji wa tovuti za serikali.

- **Kutathmini usalama wa mifumo katika Taasisi za Umma**

Idara inafanya tahmini ya usalama wa mifumo katika Taasisi za umma na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu usalama (security) kulingana na tahmini hizo

Majukumu ya Idara

- Kuaanda na kusimamia sera, kanuni na miongozo ya TEHAMA katika Utumishi wa Umma.
- Kuoanisha na kuratibu shughuli za serikali mtandao kwenye taasisi za umma kwa kuzingatia miongozo iliyowekwa.
- Kuendeleza mipango ya TEHAMA katika taasisi za umma kwa madhumuni ya kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa.
- Kuwawezesha watendaji wa Serikali katika matumizi ya TEHAMA ili kufikia hatua bora za utoaji huduma.